

**HALMASHAURI YA WILAYA NKASI**  
**MHUTASARI WA BODI YA ZABUNI-TAREHE**

28/09/2021

**AGENDA**

**AGENDA NA.01:KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 9.30 asubuhi na kuwataka wajumbe wajaadili agenda zilizokuwa mezani kwa umakini mkubwa ili waweze kutoa maazimio yatakayoleta tija kwa Halmashauri ya wilaya ya Nkasi.

**AGENDA NA.02:KUSOMA NA KUTHIBITISHA      MHUTASARI WA TAREHE**  
**10/09/2021**

Wajumbe walipitia muhutasari wa tarehe 10/9/2021 na kujiridhisha kwamba yaliyojadiliwa yalikuwa sahihi,hivyo mwenyekiti wa kikao alisaini muhutasari huo kwa ajili ya kumbukumbu ya hapo baadae.

**AGENDA NA.03:YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 10/9/2021**

NA.	AZIMIO	MHUSIKA	UTEKELEZAJI
1.	Katibu asimamie stahiki za wajumbe wa Bodi ya zabuni kwa mujibu wa sheria	Katibu wa Bodi ya Manunuzi na Ugavi	Agizo limezikatiwa.Katibu amewasiliana na Mkurugenzi Mtendaji ameahidi kulipa vikao vyote halali vya Bodi ya zabuni ambavyo ni vikao vine kwa mwaka kisheria

**AGENDA NA.05: KUOMBA IDHINI YA BODI YA ZABUNI ILI KUTUMIA**  
**SH.3,375,489,520 FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA**  
**USITAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19 KWA NJIA YA FORCE**

## **ACCOUNT/SINGLE SOURCE KATIKA UJENZI WA MADARASA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI MWAKA 2021/2022**

Kwa idhini ya Mwenyekiti katibu wa bodi ya Zabuni alieleza juu ya ujio wa fedha ya mradi wa ujenzi wa miradi ya elimu msingi na sekondari ambayo ni jumla ya sh.3,375,489,520. Kwa kutumia njia ya manunuzi ya Force account/Single source

Wajumbe walijali kwa kina juu ya ujenzi husika na kuazimia yafuatayo:

- Ujenzi huo ufanyike kwa njia ya Force account/ Single source kama ilivyo pendekezwa na Ofisi ya-Rais TAMISEMI
- Wajumbe wa bodi ya zabuni wahakikishe wanatembelea mradi ili waweze kushauri mambo mbalimbali kwa kadri mradi utakavyo kuwa unatekelezwa na siyo kutumika tu kuidhinisha njia ya manunuzi ya Force account bila kujua kinachoendelea kwenye hatua za utekelezaji.
- Wajumbe wa Bodi ya zabuni vile vile wamesisitiza sana kufuata taratibu za mwongozo wa Force Account wa May,2020 wa uundwaji wa kamati ngazi ya chini ili kuongeza uwazi na uwajibikaji.
- Wajumbe walishauri Kutoa kipaumbele kwa Taasisi za Umma katika ujenzi wa Miradi ili kupunguza gharama za usimamizi na ufuatiliaji.

### **AJENDA NA.5**

**IDHINI YA KUOMBA MATUMIZI YA SH.810,000,000 FEDHA ZA IDARA YA AFYA KWA AJILI YA UNUNUZI WA MASHINE YA X RAYS,UJENZI WA MAJENGO YA DHARURA MAANDIKO YA MIRADI NA UJENZI WA NYUMBA ZA WATUMISHI WA IDARA YA AFYA KWA NJIA YA FORCE ACCOUNT/SINGLE SOURCE 2021/2022.**

Baada ya M/kiti kutoa ufafanuzi kwa wajumbe wa bodi ya zabuni waliafikiana kwa pamoja na kutoa idhini ya kuruhusu Matumizi ya force account /Single Sourcemichakato ya maandiko iendelee kwa ajili ya maslahi mapana ya Halmashauri ya Wilaya Nkasi

Wajumbe walisisitiza uharakishwaji wa maandalizi ya makisio ya ujenzi (BOQ) ili kuharakisha utekelezaji wa shughuli za ujenzi wa miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

## AGENDA NA.06: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI

Wajumbe walimwagiza Katibu wa bodi ya zabuni kuhakikisha anakuwa bega kwa bega na kamati zitakazoundwa ngazi ya kijiji kuhakikisha zinafanya kazi kwa kuzingatia mwongozo wa Force Account/Single source

## AGENDA NA.07:KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alifunga kikao saa 10.50 asubuhi kwa kuwapongeza kwa michango yao mizuri ya mawazo ambayo hakika ni chachu ya maendeleo kwa Halmashauri ya Wilaya Nkasi,baada ya hapo aliruhusu wajumbe kuendelea na majukumu mengine.

MHUTASARI UMETHIBITISHWA/HAUJATHIBITISHWA NA:



WILLY J.NDABILA  
KATIBU BODI YA ZABUNI .....

TAREHE



MAYUMA NZILANTUZU  
MWENYEKITI BODI YA ZABUNI